

KUMB: PPR/18 - 10/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUENZIA JUMATANO, TAREHE 3 OKTOBA 2018

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika **Jumatano, Tarehe 3 Oktoba 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchini, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Septemba 2018. Kwa upande wa Mafuta ya Taa, bei za jumla na rejareja hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena mpya ya mafuta hayo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam kwa mwezi wa Septemba 2018. Kwa mwezi Oktoba 2018, bei za rejareja za Petroli zimepungua kwa Shilingi 6/lita (sawa na asilimia 0.24) wakati zile za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 32/lita (sawa na asilimia 1.39). Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimepungua kwa Shilingi 5.78/lita (sawa na asilimia 0.26) wakati zile za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 31.51/lita (sawa na asilimia 1.47). Mabadiliko haya ya bei za mafuta katika soko la ndani yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya bei za mafuta kwenye soko la dunia na gharama za uagizaji na usafirishaji wa mafuta hayo (*BPS Premium*).
- (b) Kwakuwa hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Septemba 2018, bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa mikoa ya Kaskazini hazitabadirika na hivyo bei za mwezi Septemba 2018 zitaendelea kutumika.
- (c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Mtwara zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Septemba 2018. Kwa mwezi Oktoba 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kusini** zimepungua kwa Shilingi 19/lita (sawa na asilimia 0.81) na Shilingi 16/lita (sawa na asilimia 0.69), sawia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 19.17/lita (sawa na asilimia 0.85) na Shilingi 16.20/lita (sawa na asilimia 0.72), sawia. Kupungua kwa bei za mafuta katika mikoa ya Kusini kunatokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Kwakuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zitatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi Mtwara, Lindi na Ruvuma.
- (d) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za kiganjani kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa

taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163/2018 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269/2018 la mwezi Juni 2018.****
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,368	2,304	2,247
Arusha	2,405	2,326	2,282
Arumeru (Usa West)	2,405	2,326	2,282
Karatu	2,423	2,345	2,300
Longido	2,416	2,337	2,293
Monduli	2,410	2,332	2,287
Monduli-Makuyuni	2,415	2,336	2,292
Ngorongoro (Loliondo)	2,489	2,411	2,366
Pwani (Kibaha)	2,372	2,309	2,251
Bagamoyo	2,379	2,315	2,258
Chalinze Junction	2,382	2,318	2,261
Chalinze (Msata)	2,386	2,323	2,265
Kibiti	2,388	2,325	2,267
Kisarawe	2,375	2,311	2,254
Mkuranga	2,377	2,314	2,257
Rufiji	2,395	2,332	2,274
Dodoma	2,426	2,363	2,306
Bahi	2,434	2,370	2,313

Chamwino	2,422	2,358	2,301
Chemba	2,453	2,389	2,332
Kondoa	2,459	2,396	2,338
Kongwa	2,424	2,360	2,303
Mpwapwa	2,428	2,364	2,307
Mtera (Makatopora)	2,445	2,382	2,324
Geita	2,533	2,470	2,412
Bukombe	2,522	2,459	2,401
Chato	2,554	2,491	2,433
Mbogwe	2,571	2,508	2,450
Nyang'hwale	2,548	2,485	2,427
Iringa	2,432	2,368	2,311
Ismani	2,437	2,373	2,316
Kilolo	2,436	2,373	2,315
Mufindi (Mafinga)	2,442	2,378	2,321
Kagera (Bukoba)	2,583	2,520	2,462
Biharamulo	2,558	2,494	2,437
Karagwe (Kayanga)	2,600	2,536	2,479
Kyerwa (Ruberwa)	2,605	2,542	2,484
Muleba	2,583	2,520	2,462
Ngara	2,571	2,508	2,450
Misenyi	2,592	2,528	2,471
Katavi (Mpanda)	2,576	2,512	2,455
Mlele (Inyonga)	2,558	2,494	2,437
Mpimbwe (Majimoto)	2,568	2,504	2,447
Kigoma	2,599	2,536	2,478
Uvinza (Lugufu)	2,611	2,548	2,491
Buhigwe	2,588	2,525	2,467
Kakonko	2,556	2,493	2,435
Kasulu	2,585	2,522	2,464
Kibondo	2,563	2,500	2,443
Kilimanjaro (Moshi)	2,394	2,316	2,271
Hai (Bomang'ombe)	2,398	2,319	2,275
Mwanga	2,387	2,309	2,264
Rombo (Mkuu)	2,411	2,333	2,288
Same	2,381	2,302	2,258
Siha (Sanya Juu)	2,401	2,322	2,278
Lindi	2,381	2,357	2,306
Lindi-Mtama	2,386	2,362	2,324
Kilwa Masoko	2,405	2,381	2,281
Liwale	2,417	2,393	2,327
Nachingwea	2,401	2,377	2,335
Ruangwa	2,407	2,383	2,337
Manyara (Babati)	2,439	2,360	2,316
Hanang (Katesh)	2,449	2,371	2,326
Kiteto (Kibaya)	2,454	2,376	2,331
Mbulu	2,451	2,373	2,329
Simanjiro (Orkasumet)	2,471	2,392	2,348

Mara (Musoma)	2,546	2,483	2,425
Musoma Vijijini (Busekela)	2,587	2,524	2,466
Rorya (Ingirijuu)	2,555	2,492	2,434
Rorya (Shirati)	2,590	2,526	2,469
Bunda	2,537	2,474	2,417
Butiama	2,543	2,480	2,422
Serengeti (Mugumu)	2,592	2,528	2,471
Tarime	2,557	2,494	2,436
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,562	2,498	2,441
Mbeya	2,475	2,411	2,354
Chunya	2,484	2,421	2,363
Chunya (Makongolosi)	2,499	2,435	2,378
Kyela	2,491	2,427	2,370
Mbarali (Rujewa)	2,459	2,395	2,338
Rungwe (Tukuyu)	2,484	2,420	2,363
Morogoro	2,393	2,329	2,272
Mikumi	2,408	2,345	2,287
Kilombero (Ifakara)	2,431	2,367	2,310
Kilombero (Mlimba)	2,453	2,389	2,332
Kilombero (Mngeta)	2,442	2,379	2,321
Ulanga (Mahenge)	2,441	2,378	2,320
Malinyi	2,451	2,388	2,331
Kilosa	2,411	2,348	2,290
Gairo	2,411	2,348	2,290
Mvomero (Wami Sokoine)	2,403	2,340	2,282
Turiani	2,418	2,354	2,297
Mtwara	2,368	2,344	2,319
Nanyumbu (Mangaka)	2,404	2,380	2,368
Masasi	2,384	2,360	2,345
Newala	2,388	2,364	2,351
Tandahimba	2,382	2,358	2,344
Nanyamba	2,382	2,358	2,344
Mwanza	2,518	2,454	2,397
Kwimba	2,536	2,472	2,415
Magu	2,526	2,462	2,405
Misungwi	2,512	2,449	2,391
Sengerema	2,550	2,487	2,429
Ukerewe	2,577	2,514	2,456
Njombe	2,460	2,397	2,339
Njombe (Kidegembye)	2,481	2,417	2,360
Ludewa	2,498	2,435	2,377
Makambako	2,452	2,389	2,332
Makete	2,491	2,427	2,370
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,458	2,394	2,337
Rukwa (Sumbawanga)	2,541	2,477	2,420
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,541	2,477	2,420
Kalambo (Matai)	2,548	2,484	2,427
Nkasi (Namanye)	2,554	2,491	2,433

Ruvuma (Songea)	2,453	2,429	2,370
Mbinga	2,466	2,442	2,404
Namtumbo	2,444	2,420	2,400
Nyasa (Mbamba Bay)	2,491	2,467	2,406
Tunduru	2,418	2,394	2,429
Shinyanga	2,497	2,433	2,376
Kahama	2,510	2,447	2,389
Kishapu	2,525	2,462	2,404
Ushetu (Nyamilangano)	2,528	2,464	2,407
Simiyu (Bariadi)	2,538	2,475	2,417
Busega (Nyashimo)	2,531	2,468	2,410
Itilima (Lagangabilili)	2,541	2,478	2,420
Maswa	2,530	2,466	2,409
Meatu (Mwanhuzi)	2,537	2,473	2,416
Singida	2,458	2,395	2,338
Iramba	2,471	2,407	2,350
Manyoni	2,443	2,379	2,322
Ikungi	2,454	2,390	2,333
Mkalama (Nduguti)	2,483	2,419	2,362
Songwe (Vwawa)	2,484	2,421	2,363
Songwe (Mkwajuni)	2,491	2,427	2,370
Ileje	2,488	2,424	2,367
Momba (Chitete)	2,493	2,430	2,372
Tunduma	2,488	2,425	2,367
Tabora	2,522	2,458	2,401
Igunga	2,476	2,412	2,355
Kaliua	2,541	2,477	2,420
Ulyankulu	2,535	2,472	2,414
Nzega	2,486	2,423	2,366
Sikonge	2,534	2,470	2,413
Urambo	2,535	2,472	2,414
Uyui	2,523	2,459	2,402
Tanga	2,348	2,270	2,225
Handeni	2,369	2,290	2,246
Kilindi	2,384	2,305	2,261
Korogwe	2,360	2,282	2,237
Lushoto	2,369	2,291	2,247
Mkinga (Maramba)	2,355	2,277	2,232
Muheza	2,353	2,274	2,230
Pangani	2,355	2,276	2,232

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,243.27	2,179.55	2,123.00

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,223.62	2,145.19	2,101.39

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,243.18	2,218.87	---

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA